- na mazao pia ufuta, mananasi yanaweza kupandwa katika shamba la mikorosho.
- Inashauriwa kuwa mazao kama nyonyo na mbaazi yasichanganywe pamoja na mikorosho kwa sababu yanashirikiana na mikorosho kutunza mbu wa mikorosho.

### *Faida za kuchanganya mazao*

- Kupunguza gharama za palizi
- Kupata chakula
- Kuongeza kipato
- Kuhifadhi unyevu na kupunguza joto ardhini
- Kuzuia mmomonyoko wa udongo
- Kurutubisha udongo (jamii ya mikunde)
- Masalia ya mazao mengine husaidia kulisha mifugo.



### *Kutengeneza umbile la mkorosho*

- Kutengeneza umbo la mkorosho mchanga uliobebeshwa ni kuujenga mkorosho uwe na shina na matawi ya msingi yatakayokuwa ya kudumu na yatakayozaa korosho.
- Tengeneza umbile la mkorosho uliobebeshwa wakati bado mchanga kwa kupogolea matawi yote ya chini hadi kufikia mita moja na nusu kutoka ardhini ili kuupa nafasi mkorosho kwenda juu.
- Upunguzaji wa namna hii utaupa mkorosho umbile zuri na kuwezesha palizi, kupunguza mashambulizi ya wadudu na magonjwa, kurahisisha upuliziaji wa viuatilifu na uokotaji korosho kuwa rahisi hapo baadaye.
- Matawi yote yanayoota kwa kujitandaza yapunguzwe ili kuufanya mkorosho uuote wima kuelekea juu.
- Inashauriwa kuondoa maua yanayojitokeza kwa mwaka wa kwanza ili kuuwezesha mkorosho kukua haraka.

### *Barabara za kukinga moto shambani*

- Inashauriwa kuikinga mikorosho isiathirike na moto kwa kutengeneza barabara yenye upana wa mita 3 mpaka 5 kuzunguka shamba.
- Hakikisha kuwa shamba halina magugu yanayoweza kusababisha moto kusambaa shambani.

### *Kukinga upepo shambani*

- Inashauriwa kupanda miti mpakani mwa shamba la mikorosho kukinga upepo.
- Chagua aina ya miti ambayo hukua haraka zaidi ya mikorosho na haitumii maji kwa wingi.

# MATUZO YA MIKOROSHO SHAMBANI



*Kimetayarishwa na:*

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania
TARI - Naliendele
S. L. P. 509,
MTWARA
Email : cdnaliendele@tari.go.tz

April 2019